نواقض الإسلام

Nawaaqidh al-Islaam

Mambo Yenye Kubatilisha Uislaamu

Imeeandikwa na :

Al-Imaam Muhammad ibn Abdulwahhab

Pamoja na Sharh ya :

Al-Imaam Abdulazeez ibn Baaz

Na

Shaykh al-Allaamah Abdulazeez ar-Raajihee

Manhajyasalafi.com

Yaliyomo :

Maana na Utangulizi	4
Jambo La Kwanza	5
Jambo La Pili	6
Jambo La Tatu	7
Jambo La Nne	8
Jambo La Tano	9
Jambo La Sita	10
Jambo La Saba	11
Jambo La Nane	12
Jambo La Tisa	13
Jambo La Kumi	14
Tanbihi	15

نواقض الإسلام

Nawaaqidh al - Islaam

Mambo Yenye Kubatilisha Uislaamu

Imeeandikwa na :

Al-Imaam Muhammad ibn Abdulwahhab

Pamoja na Sharh ya :

Al-Imaam Abdulazeez ibn Baaz

Na

Shaykh al-Allaamah Abdulazeez ar-Raajihee

Imefasiriwa na Abdulazeez as-Salafee

Maana Yake : [1]

النواقض Nawaaqidh : Ni wingi wa jina **ناقض**, nalo ni jina la kitu chenye kubatilisha kitu kingine ama kukitia ufisadi.

Kwa hivyo Naawaaqidhul Islaam : Maana yake ni vile vitu / ama yale mambo yenye kufasidisha na kubatilisha Uilsaamu.
Yaani mtu akifanya moja katika mambo haya; Uislaamu wake unaharibika na kubatilika – hivyo kutoka katika Dini ya Allaah na kuwa katika watu wanaoabudu vitu vengine - twajikinga na Allaah na jambo hilo. Isipokuwa aki tubia baada yake…

Utangulizi wa al-Imaam ibn Baaz [2]:

Sifa njema zote za ukamilifu ni za Allaah, na Sifa nzuri za Allaah na amani imfikie Mtume – na familia yake, na maswahaba wake, na wote wenye kufwata uongozi wake.

Ewe Muislamu juwa kwa hakika kuwa Allaah Subhanahu amewajibisha kwa watu wote waingie katika Uislaamu , na washikamane na Uislaamu, na kutahadhari na vitu vinavyokwenda kinyume na Uislaamu. Na Yeye amemtuma Mtume Muhammad sallahAllaahu alayhi wasallam kulingania watu kwa jambo hilo.

Naye Aliyetukuka amehabiri kuwa mwenye kumtii (Mtume) basi ameongoka, na hakika mwenye kumkataa basi amepotea.

Naye- katika aya nyingi- ame tahadharisha na kuritadi , na aina zote za shirk na kufr.

Na Ulamaa wametaja katika milango ya kuhusu kuritadi; kuwa muislamu anaweza kuritadi kupitia mambo mengi yenye kubatilisha Uislaamu na hivyo kuhalalisha damu na mali yake, na akawa nje ya Uislaamu.

Na katika mambo hatari zaidi katika hayo yenye kuharibu Uislaamu wa mtu ; ni mambo kumi ambayo ameyataja Shaykh al-Imaam Muhammad ibn Abdulwahhab na Ulamaa wengine – Allaah awarehemu.

Nasi tunakutajia mambo hayo kwa ujamla ; ili utahadhari, na uwa tahadharishe watu wengine kutokana na mambo haya. Vile vile tukitamani usalama na kuepukana nayo.

Hivo tunakutajia mambo haya , pamoja na ufafanuzi kidogo :

[1] Kama alivyoeleza Shaykh Abdulazeez ar-Raajihee
[2] Imaam Ibn Baaz alieleza kijitabu hiki katika Majmoo fatawaa wa maqaalat : 1

1. Kumshirikisha Allaah katika Ibaada.

Amesema Allaah Aliyetukuka kutoka na upungufu wowote:

إِنَّ اللَّهَ لا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ

"..Hakika Allaah hasamehi (dhambi ya) kushirikishwa na kitu. Lakini Yeye husamehe yasiyo kuwa hayo kwa amtakaye." [3]

Na pia Amesema :

إِنَّهُ مَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَاهُ النَّارُ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ أَنْصَارٍ

"Kwa hakika anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru." [4]

Na mifano ya hii ni: kuwachinjia majini, kuelekeza du'a na kuwaomba waliokufa , pamoja na kutaka usaidizi kupitia kwao, na kuapa , na kuwachinjia.

Shaykh Abdulazeez ar-Raajihee katika kueleza mada hii asema :

'... Ibaadaa ni jina la jumla linalo jumuisha kila tendo na kila kauli – ya dhahiri na ya siri- ambayo Allaah anayapenda.

Kwa hivyo akilekeza aina yoyote ya ibada ambayo imethubutu kwenye shariah kuwa imeamrishwa, ama imesistizwa (mustahabb) ; [akielekeza mambo haya] kwa mwengine pasi na Allaah : basi ameingia katika shirk.

Vilevile mwenye kuwacha jambo ambalo limethibitishwa katika shariah kuwa ni haraam ama ni jambo lazima kuliepuka ; [mwenye kuwacha jambo hilo] kwa sababu ya (kumridhisha) mtu mwengine pasi na Allaah ; basi amefanya shirk.

Kwa hivyo mwenye kufanya maamrisho ama kuwacha makatazo –kwa sababu ya mtu mwengine – pasi na Allaah ; basi ameeingia katika shirk...'

[3] Suratu Nisaa : 116
[4] Suratul Ma'ida : 72

2. Mwenye kufanya na kujiwekea wasila baina yake na Allaah. Akawa yuwaomba hivo viumbe vyengine na kuwaomba shaf'aa, na akawa anawategemea katika mambo yake ; basi mtu kama huyu amekufuru kwa muungano wa wanachuoni wote.

Shaykh Abdulazeez ar-Raajihee katika kueleza mada hii asema :

'.. Ni kama bile mtu kumuomba maiti aliye kaburini akasema 'yaa fulaani niombe msamaha mbele ya Allaah'

Ingawa hii inaingia katika ujumla wa shirk ; lakini hii ni hususwan. Kwani ya kwanza ni mtu kumchinjia ama kumomba ama kuapa nadhiri kwa mwengine pasi na Allaah, ama hii ya pili ni pale mtu kuweka 'wasita' baina yake na Allaah ; akifikiria kuwa hicho kitu kitafikisha maombi yake kwa Allaah. Kama vile kumwambia aliyekaburini 'ewe fulaani niombee, ama ewe mtume nisaidie,' ; hivyo amemfanya mtume kuwa baina yake na Allaah ; na hii ni shirk sababu kwa hakika atakuwa anamuomba mtu mwengine wala hamuombi Allaah. Na hakika kumuomba mwengine pasi na Allaah ni shirk na inaangia katika aya hizi :

وَلاَ تَدْعُ مِن دُونِ اللّهِ مَا لاَ يَنفَعُكَ وَلاَ يَضُرُّكَ فَإِن فَعَلْتَ فَإِنَّكَ إِذًا مِّنَ الظَّالِمِينَ

"..Na wala usiwaombe wasio kuwa Mwenyezi Mungu ambao hawakufai kitu wala hawakudhuru. Ukifanya hivyo basi utakuwa miongoni mwa walio dhulumu." [5]

Na :

فَلَا تَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ فَتَكُونَ مِنَ الْمُعَذَّبِينَ

"Basi usimwombe mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu ukawa miongoni mwa watakao adhibiwa." [6]

Mpaka aliposema (shaykh raajihee):

'...hii ni kwa sababu mwenye kuweka mtu baina yake na Allaah ; huwa kwa uhakika moyo wake unamtegemea mtu huyo na anamlemezea mambo yake mtu huyo na kumtegemea ili amtekelezee anayoyataka ; na hii ni kufr kwa Ijmaa ya waislaamu wote...'

[5] Suratu Yunus : 102
[6] Suratu Shu'araa : 213

3. Yule ambaye hawakufurishi washirikina (makafiri) , ama akawa ana shaka kuhusu ukafiri wao, au akasahihisha (na kukubali) dini zao : basi mtu kama huyu amakefuru.

Shaykh Abdulazeez ar-Raajihee katika kueleza mada hii asema :

'.. na hili neno '.. **washirikina..'** *linajumuisha makafiri wote; mayahudi, na wakristo, na wanao abudu masanamu, na wenye kukata dini... hawa wotre inawajumuisha kitu kimoja; nacho ni kumshirikisha Allaah [hivo wote wako katika kufr]*

Kwa hivyo mayahudi ni washirikina sababu hawkumuamini -mtume sallahAllaahu alayhi wasallam- na hii ni shirk, na wakristo ni mushrikun kwa vile hawkumuamini -mtume sallahAllaahu alayhi wasallam- na vile walimuabudu Isa , na wenye kuabudu masanamu ni washirikina, na majoos ni washirikina, na wanafik ni washirikina.

Kwa hivyo Yule asiye wakufurisha washirikina basi yeye amekufuru.

Na vile vile mwenye kutia shaka kuhusu ukafiri wa makafiri; yaani aliye na shaka kuwa yahudi ni kaafir, au nasara ni kaafir , au mwenye kuabudu sanamu ni kaafir ; basi mtu huyo ni kaafir sababu ya shaka hii.

'..au akasahihisha (na kukubali) dini zao..' : *Kwa kusema kuwa mayahudi ama manasara wako katika dini ya sawa, au anapouulizwa kuhusu mayahudi na manaswara anasema 'mimi sisemi kitu kuhusu wao, mayahudi wako kwenye dini, na manaswara wako kwenye dini, na waislamu wako kwenye dini ; hivyo mwenye kupenda kufwata dini ya uislamu ama mayahudi ama manaswara basi chaguo ni vile anavyopenda' : hakika mwenye kusema hivyo ni kaafir kwa Ijmaa, sababu yenye ameswahihisha mienendo ya washirikina, na sababu yeye hawakufurishi washirikina...'*

4. Mwenye kuitakidi kuwa kuna muongozo mwengine ambao ni bora kuliko muongozo wa Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam.

Au kuitakidi kuwa kuna hukmu nyengine ambayo ni bora kuliko hukmu ya Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam ; kama wale wanao fadhilisha hukmu za tawaagheet [7] kuliko hukmu yake : basi mtu huo (mwenye kuitakidi hivi) ni kaafir.

[7] Tawaagheet ni wingi wa twaaghoot ; ambayo maana yake ni mtu ama kitu chochote kinacho abudiwa – pasi Allaah – hali ya kuwa mtu/kitu hicho kinaridhika na kuabudiwa huko.

Katika kueleza mada hii , Al-Imaam Ibn Baaz asema :

Na inaingia katika hii :

- Mwenye kuitakidi kuwa kaanuni na shariah zilizotungwa na binaadamu ; kuwa ni bora kuiko Shariah ya kiislaamu,

- au kuwa ni sawa na Shariah ya kiislaamu ,

-au kuitakidi kuwa inafaa kuhukumu na kaanuni hizo ; basi huyo amekufuru.

Hata ikiwa ana itakidi kuwa Shariah ya kiislaamu ndio bora. [maadamu anaitakidi kuwa inafaa kuhukumu na kaanuni hizo ; basi huyo amekufuru.]

- au mwenye kutakidi kuwa Shariah ya kiislaamu si sawa kutumiwa katika karne ya ishirini (20th century).

- au mwenye kutakidi kuwa Shariah ya kiislaamu ndiyo sababu ya kufarikisha waislaamu

- au mwenye kutakidi kuwa Shariah ya kiislaamu inatosheleza kuwa katika mambo ya baina ya mja na Allaah (yaani katika ibaada) pekee ; wala si lazima iwekwe katika mambo yote ya ki maisha.

-Na vilevile : Mwenye kuona kuwa kutekelezwa kwa hukmu ya kukatwa mwizi mkono, ama kupigwa mawe mzinifu : haina usawa katika wakati wa sasa

-Na pia mwenye kuitakidi kuwa yafaa kutumia hukmu nyengine pasi na hukmu ya Allaah katika mienendo ya kila siku, na katika hadd [8] , ama katika mambo mengine ; basi mtu mwenye kuitakidi hivi amekufuru pia ; hata kama yeye haitakidi kuwa hukmu hizi nyengine ni bora kuliko hukmu ya Shariah ya Allaah. Hii ni kwa sababu kuitakidi hivo, yeye atakuwa ame halalisha ambayo Allaah ameharimisha –

-Na pia mwenye kuhalalisha yanayojulikana kwa Ijmaa kuwa ni haramu ; kama zinaa, na kuhukumu na shariah nyengine pasi na Shariah ya Allaah, na ribaa, na pombe; amekufuru.

Twamuomba Allaah atuongoze sote tufanye yale yanayomridhisha Yeye, na atuongoze sisi na waislaamu wote katika Siraatul Musataqeem, Hakika Yeye ni Mwenye Kusikia, Aliyekaribu kujibu maombi.

[8] Hadd ni zile adhabu zinazotekelezwa kisheria , kama kupigwa mawe wazinifu, na kukatwa mkono mwizi..

5. Mwenye kuchukia kitu chochote alichokuja nacho Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam – hakika amekufuru. Hata kama mtu huyo anakifanya kitendo hicho.

Kulingana na kauli Yake :

ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَرِهُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ

"Hayo ni kwa sababu waliyachukia aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi akaviangusha vitendo vyao (wakawa hawana thawabu hata za amali walizofanya)." [9]

Shaykh Abdulazeez ar-Raajihee katika kueleza mada hii asema :

'..Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam ametumwa na Sharia yenye swala na zakah, na shariah ya kuowa mke zaidi ya mmoja ; hivyo mwenye kuchukia kitu katika hukmu hizi za Shariah ama hukmu zozote nyengine alizotumwa nazo Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam; basi amekufuru.

Na hivyo inalazimika kuwa fahamisha wanawake kuwa haifai kuchukia hukmu ya 'kuowa mke zaidi ya mmoja' ; kwa sababu ni hukmu ya Allaah na mtume Wake.

Lakini ikiwa mwanamke ana karaha ya kimaumbile kuhusu jambo hili – wala si chuki na kukataa jambo hili la Shariah ; basi hii haidhuru , ama kama vile kwa sababu wanaume wengine hawatimilizi uadilifu ; hivyo akawa yeye mwanamke ana karaha kwa mwanamume asiongeze mwanamke mwengine –kwa sababu hii- basi haina neno (wala haitokuwa ni kufr)

Ama kukataa na kuchukia hukmu wenyewe ya Shariah basi huku ni kuritadi, ama kuchukia mambo mengine katika swala ama zakaah, ama sawm, ama hajj ; basi hii ni kufr...'

[9] Suratu Muhammad : 9

6. Mwenye kufanyia istihzai kitu chochote katika dini aliyokuja nayo Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam , au kufanyia istihzai thawabu au adhabu ya jambo aliyokuja nalo : basi amekufuru.

Na dalili ni Kauli Ya Allaah :

وَلَئِن سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ لا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ

"Na ukiwauliza (kwa nini wanaifanyia mzaha dini), wanasema: Sisi tulikuwa tukipiga porojo na kucheza tu. Sema: Mlikuwa mkimfanyia maskhara Mwenyezi Mungu na Aya zake na Mtume wake?

Msitoe udhuru; mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu!" [10]

Shaykh Abdulazeez ar-Raajihee katika kueleza mada hii asema :

'.. akifanyia istihzai swala basi amekufuru, akifanyia istihzai zaka basi amekufuru, akifanyia istihzai sawm basi amekufuru, akifanyia istihzai ndevu basi amekufuru; sababu kuchukia na kukirihika na ndevu ni kukirihika na amri iliyokuja katika Usilaamu kuamrishwa kueka ndevu kupitia kauli ya Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam; hivyo atakuwa amekufuru. Ama kufanya istihzai kuhusu dhati ya mtu ama tabia yake wala si istihzai ya hukmu ya shariah – basi hii si kufr.

Na vile vile kufanyia istihzai pepo kama kusema: 'vipi hio pepo? Hio pepo ni jaza ya waumini ehh!..' anafanyia mzaha hio. Ama kufanyia istihzai adhabu ya moto na kusema : 'moto ni adhaabu ya makafiri eeh!' kufanya mzaha na istihzai ; huku ni kukufuru – na tunaomba kiinga kutoka na Allaah na mambo haya..'

[10] Suratu Tawba : 65-66

7. Uchawi ; na inajumuisha Swarf na 'Atf.[11]

Hakika yeyote mwenye kuufanya uchawi, au yeyote mwenye kuridhika nao ; basi amekufuru.

Na dalili ni Kauli Ya Allaah :

وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّى يَقُولا إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلا تَكْفُرْ

'....Wala hao (Malaika) hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani (kuangalia kutwii kwenu); basi usikufuru.' [12]

Asema Shaykh ar-Raajihee :

Swarf : ni ule uchawi unaofanywa kufarikisha mtu na mkewe; nayo athari yake ni mume akawa amuona mkewe kwa sura mbaya hivyo akamuepuka, naye mke humuona mumewe katika sura mbovu hivyo akakaa mbali naye.

Atf : ni ule uchawi ambao ni kinyume cha swarf; yaani ni uchawi unaofanywa kuleta mafungamano baina ya mke na mume, hivyo akamuona ni mzuri ki maumbile au kitabia hali ya kuwa ni muovu.

11

Kwa ufafanuzi mzuri wa mada hii ya uchawi na wachawi ; tafadhali sikiza kanda za Shaykh Nassor : http://www.qssea.net/audio_index.htm

12 Suratul Baqarah : 102

8. Kuwasaidia washirikana (makafiri) na kuwapa nguvu dhidi ya waislaamu.

Na dalili ni Kauli Yake :

وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنْكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

"…Na miongoni mwenu atakaye fanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi (njia ya kheri) watu madhalimu." [13]

Shaykh Abdulazeez ar-Raajihee katika kueleza mada hii asema :

'..maana yake ni kuwasaidia washirikana kama vile ikiwa kuna vita baina ya waislaamu na makafiri ; ikawa anasaidia makafiri dhidi ya waislaamu kwa kupitia kitu chochote. Aidha kuwasaidia kwa mali , silaha, au kwa rai.

Hivyo akiwasaidia atakuwa amekufuru; kwa sababu ame wapa fadhlaa na daraja washirikina juu ya waislaamu; na jambo hili lina lazimu kuwa ana chuki kwa Uislaamu na Allaah na mtume ; na hii ni kufr na kuritadi….'

Mpaka aliposema :

'… na kuna tofauti baina ya kuwapa usaidizi na baina ya kushirikiana nao ; yaani kuwapa usaidizi na kuwapenda dhidhi ya waislaamu ; hii ni kufr. Ama kushirikiana katika mienendo yao na kuwafanya marafiki (bila ya kuwa saidia dhidi ya waislaamu) ; hii ni katika madhambi makubwa wala si kufr.'

[13] Suratul Maidah : 51

9. Kuitakidi kuwa kuna watu fulani ambao wao inafaa kwa wao kuwa nje ya shariah aliyotumwa nayo Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam.

Mwenye kuamini kitu kama hicho (kuwa si lazima kwa mtu/watu Fulani kufwata maamrisho ya Allaah) ; basi ni kafiri.

Kulingana na Kauli ya Allaah :

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ

"..Na anaye taka dini isiyo kuwa Uislamu; haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye hasara." [14]

Shaykh Abdulazeez ar-Raajihee asema :

'.. hivyo yeyote mwenye kuitakidi kuwa yafaa kwa mtu kutoka kwenye shariah aliyotumwa nayo Muhammad sallahAllaahu alayhi wasallam – na hivyo kuabudu kwa shariah zengine; basi huyu ni kaafir.

Kwa nini?

Sababu shariah aliyotumwa nayo Muhammad sallahAllaahu alayhi wasallam – ni Shariah ya jumla ; kwa binaadamu , majini, waaraabu, na wasio waarabu.

Na pia sababu Shariah hii imefuta na kuondoa shariah zote zengine

Na pia sababu baada ya kutumwa Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam; imekuwa shariah hii ndio inayostawi kwa vitu vote hadi siku ya Qiyamah...'

Kauli ya Allaah :

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

"Sema (ewe Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam): 'Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote.." [15]

[14] Suratul Aali Imraan : 85
[15] Suratul A'araaf : 158

10. Kuipa mgongo dini ya Allaah ; akawa hatafuti Ilimu ya dini , na wala hafanyi vitendo .

Na dalili ni Kauli ya Allaah :

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ ذُكِّرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ ثُمَّ أَعْرَضَ عَنْهَا إِنَّا مِنَ الْمُجْرِمِينَ مُنْتَقِمُونَ

"Na ni nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye kumbushwa kwa Aya za Mola wake, kisha akazikataa? Hakika Sisi ni wenye kuchukuwa kisasi kwa wale wabaya."[16]

Shaykh Abdulazeez ar-Raajihee asema :

'..Kuipa mgongo dini ya Allaah ; akawa hatafuti Ilimu ya dini , na wala hafanyi vitendo ... : hichi kitendo ni chenye kubatilisha Uislaamu.

Kwa hivyo yule ambaye ameipa mgongo dini ya Allaah ; hamuabudu Allaah, wala hatafuti ilimu ya dini ; huyu ni kaafir. Sababu katika hali hii yeye ni katika wale wanaomuabudu shaytani. Sababu hakuna mtu isipokuwa ana abudu na ana kitu anacho kiabudu ; hivyo – yule ambaye hamuabudu Allaah huwa anamuabudu shaytani.

Na huyu ndio katika wale ambao watu husema kuhusu wao 'hawa hitaji dini' : hasomi dini wala hamuabudu Allaah , huyu hakika anamuabudu shaytani kwa sababu shaytani ndiye anayemuamrisha kufanya hivo.

Kwa hivyo huyu ambaye anaye jiona kuwa hataki kuelewa dini ya Allaah wala kumuabudu Allaah; huwa amemtwii shaytani , hivyo akawa anamuadu shaytani. Hivyo yoyote ambaye hasomi dini ya Allaah wala hamuabudu Allaah kwa kitendo hata kimoja – si dua, wala haswali, wala hana mapenzi ya Allaah, wala hana ibada za matamshi, wala Imani, wala haitakidi kuwa Allaah ndiye Al-Khaaliq (Muumba wa kila kitu) , Ar-Raaziq (Mwenye riziqi za kila kitu), al-Mudabbir (anayepeleka mambo yote), wala haamini kuwa Allaah ndiye apasaye kuabudiwa kwa haki : basi mtu huyu ni kaafir kwa huku kukana na kukataa kwake.'

[16] Suratul Sajda : 22

Na hakuna tofauti katika haya mambo; kwa mwenye kuyafanya hali ya kuwa ni mzaha, au bila ya mzaha (yaani kwa kutaka), au kwa kuogopa. [yote ni kufr]

Isipokuwa kwa mwenye kuzifanya hali ya karaha (yaani kulazimishwa).

Na yote haya ni katika mambo hatari kabisa , nayo ni katika mambo yanoyofanyika sana.

Kwa hivyo inatakikana kwa Muislamu kutahadhari na kuogopea nafsi yake asije akaiingilia mambo haya.

Tunajikinga na Allaah kutokana na ghadhabu yake na adhabu yake kali.

Sifa nzuri za Allaah na amani zimfikie kiumbe bora zaidi – Muhammad – na familia yake, na maswahaba wake.

Shaykh Abdulazeez ar-Raajihee asema :

'.. kwa hivyo tuna hali tofauti :

- Mtu anafanyina mzaha dini kwa kejeli na istihzai tu! Mfano anafanyia istihzai swala, ama dini ; anafanya mzaha na istihzai, jee anakufuru?

Jawabu ni : Naam.

- mtu anafanyia istihzai dini kwa kutaka wala si mzaha ; huyu ana kufuru.

- mwengine anafanya jambo katika haya mambo (10 yaliyotajwa) hali ya khofu ya nafsi yake ama mali yake ama mtoto wake ; huyu anakufuru sababu amefanya jambo la kubatilisha uislaamu. Anaitukana dini mbele ya mtu kwa sababu ya kuogopea mali yake isipotee , sababu anaona asipotukana dini mali yake itachukuliwa, anaogopea mali yake ama nafsi yake, ama mtoto wake ; jee anakufuru? Ndio.

Kwa hivyo mwenye kufanya haya mambo yenye kuharibu Uislaamu – sawa kwa mzaha, au bila ya mzaha, au kwa khofu; anakufuru. Isipokuwa mtu anayefanya hayo hali ya kuwa katika ulazimisho; na sharti ya kuwa moyo wake umetulia katika Imaan.

Ama moyo wake ukikubali kufr pia ; basi yeye hukufuru pia.

Mfano ni mtu amewekewa panga ; kufuru ama tutakuuwa!

Huyu akitamka kufr hali ya kuwa moyo wake umetulia katika Imaan; basi hakufuru. Ama mwenye kufanyiwa hivyo hivyo akatamka kauli ya kufr hali ya kuwa moyo wake umekubali na kuamini kufr hiyo ; basi huyo amekufuru.

Kwa hivyo tuna hali tano :

1. Amefanya kufr ama moja katika haya mambo ya kuharibu Uislaamu ; kwa mzaha na istihzai – huyu anakufuru

2. Amefanya kufr ama moja katika haya mambo ya kuharibu Uislaamu ; kwa kutaka – huyu anakufuru

3. Amefanya kufr ama moja katika haya mambo ya kuharibu Uislaamu ; kwa khofu - huyu anakufuru

4. Amefanya kufr ama moja katika haya mambo ya kuharibu Uislaamu ; kwa kulazimishwa ; akafanya hivyo kwa kukubali na kuamini kufr hiyo moyoni mwake – huyu anakufuru

5. Amefanya kufr ama moja katika haya mambo ya kuharibu Uislaamu ; kwa kulazimishwa ; akafanya hivyo hali ya kuwa Imaani ya Uislaamu imejaa moyoni mwake – huyu Hajakufuru.

Kwa hivyo hizo hali tano, nne anakufuru ila moja. Dalili iko wapi? Maanake watu wengine waweza kusema; hata huyu aliyekufuru kwa kuogopea nafsi yake ama mali yake au ahli yake – hivyo akatamka kalima za kufr sababu ya khofu ili mali yake ibake?

Twasema hii ni kufr kama Alivyosema Allaah :

مَن كَفَرَ بِاللّهِ مِن بَعْدِ إِيمَانِهِ إِلاَّ مَنْ أُكْرِهَ وَقَلْبُهُ مُطْمَئِنٌّ بِالإِيمَانِ

“Anaye mkataa Mwenyezi Mungu baada ya kuamini kwake - isipo kuwa aliye lazimishwa na hali ya kuwa moyo wake umetua juu ya Imani,[17]

Kwa hivyo Allaah ametoa udhuru ya hali moja ; naye ni Yule aliyelazimishwa, na iwe kwa sharti : kuwa moyo wake :

إِلاَّ مَنْ أُكْرِهَ وَقَلْبُهُ مُطْمَئِنٌّ بِالإِيمَانِ

“Anaye mkataa Mwenyezi Mungu baada ya kuamini kwake - isipo kuwa aliye lazimishwa na hali ya kuwa moyo wake umetua juu ya Imani,

Kisha (katika aya inayofuata) akasema Allaah :

[17] Surau Nahl : 106

وَلَـــكِن مَّن شَرَحَ بِالْكُفْرِ صَدْرًا فَعَلَيْهِمْ غَضَبٌ مِّنَ اللّهِ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ذَلِكَ بِأَنَّهُمُ اسْتَحَبُّواْ الْحَيَاةَ الْدُّنْيَا عَلَى الآخِرَةِ وَأَنَّ اللّهَ لاَ يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ

'..lakini aliye kifungulia kifua chake kukataa - basi hao ghadhabu ya Mwenyezi Mungu ipo juu yao, na wao watapata adhabu kubwa.

Hayo ni kwa sababu wameyapenda zaidi maisha ya duniani kuliko ya Akhera, na kwa sababu Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri." [18]

Na kulazimishwa ; ni kule kuwekwa chini ya vizuizi ; yaani akawa amelazimishwa kwa kuwekewa upanga katika shingo yake....

Kwa hivyo moyo wake ukituwa katika Imaan ; basi haitomdhuru kauli hiyo ya au kitendo hicho cha kufr. Amma kuwa na hofu tu ya kawaida -kwa mali yake au ahli yake (bila ya kulazimishwa na kukirihishwa kama kuwekewa upanga); basi hii hai halalishi kufr; na atakuwa amekufuru.

Twamuomba Allaah usalama na uzuri, na tunijikinga kwake na shirk na kufr na unafiki na tabia mbovu.

Twamuomba Allaah Subhanahu atufishe katika Uislaamu,

Twamuomba Allaah Subhan atu thabitishe katika Dini yetu,

Na Atukinge na fitna na mapotevu,

Tusiwe wenye kubadilika wala kukengeuka,

Hakika Yeye ndiye Muweza wa kututekelezea mambo hayo ;

na Sifa nzuri za Allaah na amani imfikie Mtume – na familia yake, na maswahaba wake, na wote wenye kufwata uongozi wake.

[18] Suratu Nahl : 106-107